za vipodozi zinazotengenezwa na Kampuni ya Oriflame Tanzania kwa kutumia malighafi za asili ikiwemo mimea, matunda na maua.

"Biashara inayohusu urembo siyo ya akinamama na akinadada pekee hata akinakaka na akinababa pia wanaweza kufanya kwani bidhaa hizi ni kwa watumiaji wote wa kike na wa kiume, hivyo napendekeza wenzetu wajiunge kwa wingi pia ili kujikwamua kiuchumi" alisema.

Alisema kuwa watu wengi wamekuwa wakiona biashara ya kusambaza vipodozi ni kama umachinga kutokana na kuhitaji kuzunguka kutafuta wateja na kushawishi watu kujiunga kununua bidhaa. Aliwataka kutokata tamaa kwa kuwa mtu anapojituma biashara hiyo huwa na faida kubwa.

Meneja Masoko wa Oriflame Tanzania, Fortunata Nkya alisema kuwa tangu kampuni hiyo ilipoanza kufanya kazi nchini mwaka jana mpaka sasa imeshaajiri Watanzania zaidi ya 7,000 na hivyo kuwasaidia kuondokana na umasikini wa kipato.



# Vikwazo vya biashara kufanyiwa masihara na wachora vibonzo

**Na Mwandishi wetu**

JUMUIYA tatu kubwa za kibiashara nchini, Ijumaa wiki hii zitazindua ripoti ya mtazamo wa wafanyabiashara kuhusu mazingira ya biashara Tanzania.

Uzinduzi huo utaambatana na maonesho ya vibonzo kuhusu mazingira hayo na kuanzwa kwa kipindi kipya cha redio cha 'Wacha Masikhara!' Kinachofanyia masikhara masuala yanayokwaza ustawi wa kibiashara na kiuchumi Tanzania.

Jumuiya zinazohusika katika uzinduzi huo ni Shirikisho la Biashara na Viwanda (CTI), Shirikisho la Utalii Tanzania (TCT) na Jumuiya ya Vikundi vya Biashara Ndogondogo (VIBINDO).

Kwa mujibu wa taarifa uzinduzi huo utafanyika Nafasi Art Space, Mikocheni jijini Dar es Salaam.

"Umma, ikiwa ni pamoja na watendaji wa biashara, watapata fursa ya kuburudika na masihara kuhusu vikwazo vya biashara nchini Tanzania na kutafakari hatua za kuchukua," alisema Mwenyekiti wa VIBINDO, Gaston Kikuwi.

Ripoti itakayozinduliwa inaitwa "Mitizamo ya Viongozi wa Biashara Juu ya Mazingira ya Uwekezaji Tanzania – 2011". Ripoti hiyo ndiyo imewachagiza wachoraji wa vibonzo vitakavyokuwa kwenye maonesho.

Ripoti hiyo, ambayo imeandikwa na mshauri mwelekezi wa Uingereza, David Irwin, hutolewa kila mwaka na Kitengo cha Utetezi cha Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (Business Environment Strengthening for Tanzania Programme-Advocacy Component, BEST-AC).

**Na Namsembaeli Mduma, Kiteto**

UFUATILIAJI na usimamizi wa utekelezaji wa utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kutumia vocha wilayani hapa, umesuasua kwa misimu miwili mfululizo kutokana na ukosefu wa fedha, kwa shughuli hiyo.

Ofisa Kilimo Mwandamizi, Robert Urasa na Mratibu wa pembejeo katika Wilaya ya Kiteto, Lioba George, walitoa taarifa hiyo kwa watumishi waliofika kufanya tathmini ya shughuli hiyo kutoka makao makuu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Walisema tangu walivyowezeshwa kifedha mwaka 2009/10, hawajakumbukwa tena. Kwa mujibu wa Urasa, wamekuwa wakilazimika kutumia fedha za ofisi yao zilizopangwa kwa ajili ya matumizi mengine, ili kufanya ufuatiliaji na usimamizi huo katika maeneo machache ya vijiji vya wilaya hiyo.

Kutokana na maelezo hayo, Ofisa kutoka wizarani, Dorcas Shempemba aliwataka wawe makini na akaunti wanazozitoa kwa ajili ya kutumiwa fedha hizo kwa kuwa uzoefu unaonesha kuwepo kwa wilaya zinazotoa akaunti zilizofungwa au za watu wasiohusika na hivyo kusababisha fedha zipotee.

Kwa upande wake, George alisema wanasumbuliwa na changamoto ya kupata taarifa wanazohitaji kutoka

kwa ajili ya kufanya ulinganisho kwa kuwa wahusika wa benki hiyo wanataka kupata maelekezo kutoka makao makuu ndipo wawape ushirikiano.

Hata hivyo George alisema walipokea vocha 5555 za pembejeo za ruzuku kwamsimu wa 2011/12 zilizotumika zote na kuvinufaisha vijiji 39 vilivyosambaziwa bidhaa hizo na mawakala watano. Hadi kufikia Juni 12, mwaka huu, NMB ililipa vocha 4399 za mbegu.